

"Achieving consensus on the science of food regulations and legislation to ensure the global availability of safe and wholesome food products for all consumers"

MAWASILIANO NA VYOMBO VYA HABARI: Timu ya mawasiliano ya GHI
communications@globalharmonization.net

KWA KUTOLEWA HARAKA

**HAKUNA KISINGIZIO CHA KUTOTOA TAARIFA YA MATUKIO
YA UKIUKWAJI USALAMA WA CHAKULA POPOTE
YANAPOTOKEA DUNIANI**

Tovuti ya watoa taarifa ya matukio ya ukiukwaji usalama wa chakula iliyopo kwenye lugha mbalimbali itasaidia yeyote anayefanya kazi kwenye sekta ya chakula na vinywaji popote duniani kutoa taarifa ya matukio ya ukiukwaji usalama wa chakula bila kujulikana.

(Viena, Austria) Desemba 1, 2021 - GHI inapenda kutangaza kwamba tovuti ya watoa taarifa ya matukio ya ukiukwaji usalama wa chakula ipo na kwa zaidi ya lugha 30. Inapatikana hapa: <https://whistle.globalharmonization.net> kwa yeyote aliyeko nchi yoyote, ambaye anafanya kazi kwenye sekta ya chakula na vinywaji.

Mpaka sasa hakujawahi kuwepo na mfumo wa kiulimwengu wa kutoa taarifa za wasiwasi kuhusu usalama wa chakula, bila mtoa taarifa kujulikana. Ili kukabiliana na tatizo hilo, GHI imeanza kwa kuzindua tovuti ya watoa taarifa ya matukio ya ukiukwaji usalama wa chakula mwezi Agosti mwaka 2021. Kusudi la kutoa taarifa katika tovuti hii ni ili taarifa hizo ziwe kizuizi kwa wasambazaji chakula wasio waaminifu.

Hakutakuwepo tena na kisingizio cha kutotoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa usalama wa chakula ambao unaweza kuwadhuru walaji, kuwafanya wagonjwa ama kuwasababishia vifo. Kwa hivyo tunawahimiza watu wanaofanya kazi kwenye viawanda vya vyakula na vinywaji, popote pale duniani kutoa taarifa juu ya wasiwasi wowote walio nao kuhusu usalama wa chakula wanachozalisha.

Je, utaruhusu familia yako ile chakula unachozalisha katika kiwanda ama sehemu unakofanyia kazi? Kama jibu ni hapana, kwa nini? Je, kinasababisha majanga ya kiafya kwa watu watakaokula chakula hicho? Kama jibu ni ndio, basi sasa una njia ya kutoa hii taarifa bila kujulikana.

Tovuti ya kutolea taarifa kwa lugha zaidi ya 30 ni hii hapa: <https://whistle.globalharmonization.net/>. Kwa yeyote anayeamua kutoa taarifa ya tukio la ukiukwaji wa usalama wa chakula katika tovuti hii anahakikishiwa kwamba hatojulikana na kwamba hata GHI yenyewe haitajua ni nani aliyetoa taarifa. Hii ni njia madhubuti ya kumlinda na kutotambulikana kwa mtoa taarifa.

Kama ilivyoielezwa kwenye tovuti, sehemu ya “Maswali yaulizwayo mara kwa mara” kuna taratibu/kanuni rahisi ambazo mtoa taarifa anaweza kuzifuata (Angalia <https://whistle.globalharmonization.net/faq>). Kwa mfano, usitumie vifaa vya kampuni kama vile simu ama kompyuta au mtandao wa kampuni kujaza fomu. Tumia kurasa binafsi (private pages) za *kivinjari kisichojulikana* (browser incognito) na usitaje chochote kinachoweza kufanya ujulikane. Kwa njia hii unaweza kuwa salama kwa kulinda utambulisho wako.

Now available in over 30 languages for food industry workers wherever they are <https://whistle.globalharmonization.net>

Would you let your family eat the food you make at work?

¿Permitiría Ud. que su familia consuma el alimento que Ud. produce en su trabajo?

Bạn có cho gia đình mình ăn những thực phẩm bạn làm việc không?

هل تسمح لأسرتك أن تأكل من الطعام الذي تصنعه في العمل؟

您会让您的家人食用在您的公司中制作的食物吗?

Позволите ли вы своей семье потреблять продукцию, которую производит Ваше предприятие?

Կըթոյաւորե՞ք ձեր ընտանիքի անդամներին պատրաստել եւ աշխատավայրում






GHI Whistleblower Food Safety Incident Report Site

هل تسمح لأسرتك أن تأكل من الطعام الذي تصنعه في العمل؟

Would you let your family eat the food you make at work?

Bạn có cho gia đình mình ăn những thực phẩm bạn làm việc không?

あなたの家族にあなたが職場（食品工場）で作った食品を食べさせますか？

¿Permitiría Ud. que su familia consuma el alimento que Ud. produce en su trabajo?

您会让您的家人食用在您的公司中制作的食物吗？

Позволите ли вы своей семье потреблять продукцию, которую производит Ваше предприятие?

ඔබවිසින් රැකියා ස්ථානයේදී පිළියෙල කරන ආහාර ඔබේ පවුලේ සාමාජිකයන්ට පරිභෝජනය කිරීමට දීමට තරම් එහි ප්‍රමිතිය ඔබට විශ්වාසදායකද?











GHI Whistleblower Food Safety Incident Report Site

Would you let your family eat the food you make at work?



Facebook:GHI4FoodSafety**Twitter:** @GHI4FoodSafety**LinkedIn:**global-harmonization-initiative

###